

Habari Leo Jumanne Machi 31, 2026 Pg 3

Fedha za SGR zaipa tuzo Tanzania

Na Mwandishi Maalumu

SERIKALI ya Tanzania imeshinda tuzo ya kimataifa ya fedha za miundombinu mwaka 2026.

Imeshinda tuzo hiyo kwa kuzingatia mafanikio ya upatikanaji wa mkopo wenye masharti nafuu wa Dola za Marekani bilioni 1.78 kugharimia ujenzi wa Reli ya Kisasa ya Umeme (SGR) kwa kipande cha tatu na cha nne.

Kaimu Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Rished Bade amepokea tuzo hiyo kwa niaba ya Wizara ya Fedha katika hafla ya utoaji tuzo za kimataifa za benki na masoko jijini Cape Town, Afrika Kusini.

Ushindi huo unatokana na mpango wa utafutaji ufadhili wa mradi huo wa kinkakati unaotarajiwa kuchochea ukuaji wa uchumi na kurahisisha usafirishaji nchini na Ukanda wa Maziwa Makuu.

Mkopo huo ulipatikana kwa ushirikiano kati ya taasisi za bima za nchi za Sweden, Poland na Italia na benki za maendeleo za kikanda kwa uratibu wa Benki ya Standard Chartered.

Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk Natu Mwamba wamesema tuzo hiyo inatokana na maelekezo na uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu usimamizi

wa Deni la Serikali na upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu.

"Tuzo hii ni ushindi unaendelea kuiweka Tanzania katika nafasi nzuri kwenye masoko ya fedha ya kimataifa, ukiakisi uwezo wa nchi kubuni na kutekeleza mikataba mikubwa ya kifedha kwa ajili ya miradi ya kinkakati ya maendeleo pamoja na kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi," alisema Balozi Omar.

Tuzo za kimataifa za benki na masoko zimekuwa zikitolewa tangu mwaka 2014 ili kuzitambua nchi na taasisi zilizofanikiwa kuingia mikataba bora ya kifedha kupitia masoko ya mitaji na mikopo.

Vigezo vinavyozingatiwa ni

ubunifu wa muundo wa kifedha, unafuu wa masharti ya mikataba na ubora wa utekezaji wa mipango ya ufadhili wa miradi husika.

Hivi karibuni Tanzania ilipata ushindi wa jumla wa mwaka katika tuzo za Jumuiya ya Madola za usimamizi wa deni la umma.

Pia, Tanzania ilitwaa Tuzo ya Ofisi Bora Kanda ya Afrika kupitia Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali katika Wizara ya Fedha.

Tuzo hizo zilitangazwa Machi 26, mwaka huu wakati wa mkutano wa Jukwaa la Jumuiya ya Madola kuhusu usimamizi wa deni la umma uliofanyika jijini London, Uingereza.